# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MIUNDOMBINU, ARDHI NA TEHAMA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAWASILIANO, TEKNOLOJIA YA HABARI NA UBUNIFU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa unyenyekevu, naomba nianze kwa kumshukuru **Mwenyezi Mungu**, muweza wa yote kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana hapa siku ya leo kwa lengo la kujadili Utekelezaji wa Makadirio ya Matumizi na Mapato ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mapendekezo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** pamoja na Makamu wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza Nchi hii, pamoja na jitihada

anazozichukua katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi na kuhakikisha analeta maendeleo na mabadiliko ya kasi nchini kwa kuweza kuunda Wizara hii mpya ili kurahisisha huduma za mawasiliano na masuala ya Ubunifu.

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba nikushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid** Spika wa Baraza la Wawakilishi, na **Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma** Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na **Wenyeviti wa Baraza** kwa umahiri na uzoefu wenu mkubwa mnaotumia kuliongoza Baraza hili kwa uweledi na uhodari wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Sina budi pia kumshukuru Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu Zanzibar, **Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga,** pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa **Mohamed Sijamini Mohamed,** Katibu Mkuu, Naibu katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa mashirikiano waliyotupatia Kamati yetu wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara yao.

**Mheshimiwa Spika,** Shukran za pekee nazitoa kwa Wajumbe wa **Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA** ambao kwa pamoja tumeweza kujadili kwa kina mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha

zinazoidhinishiwa zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na kuleta ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Heshima kubwa Naomba niwatambulishe Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mihayo Juma N'hunga | Mwenyekiti, |
| 2. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | M/Mwenyekiti, |
| 3. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe, |
| 4. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe, |
| 5. | Mhe. Khamis Mohammed Amran | Mjumbe, |
| 6. | Mhe. Abdullah Kambotwe Abdullah | Mjumbe, na |
| 7. | Mhe. Said Ali Mbarouk | Mjumbe. |

**Aidha,** Kamati yetu inafanyakazi na makatibu wasaidizi ambao wamekuwa muhimili muhimu sana katika kutekeleza majukumu yetu. Makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1) | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu, |
| 2) | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu, na |
| 3) | Ndg. Adam Maulid Simai | Afisa Bajeti. |

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka.

Hivyo, katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa na kanuni ya 101 fasili ya kwanza, Kamati ilikaa, kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Mawasiliano, Teknologia ya Habari na Ubunifu kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu imetekeleza kazi zake kupitia Programu Kuu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo ilikua chini ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, ambapo kwa Mwaka huu wa fedha 2026/2027 Wizara hii mpya ya Mawasiliano, Teknologia ya Habar na Ubunifu ina fungu lake moja ambalo ni **059** na imepanga kutekeleza **Programu Kuu Tatu (3) zenye Programu Ndogo Sita (6) ambapo** kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara hii ya Mawasiliano, Teknologia ya Habari na Ubunifu kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hizo ni **Shilingi Bilioni Hamsini na Tatu, Milioni Mia Tatu Tisiini na Moja na Laki nane (53,391,800,000/-)** kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu, inasimamia Taasisi mbili zinazojitegemea ambazo ni **Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA)** na **Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ)** ambapo awali Taasisi hizi zilikua katika

Wizara nyengine kabla ya kuundwa kwa Wiizara hii mpya. Kutokana na umuhimu wake na kwenda sambamba katika kupiga hatua kwenye masuala mazima ya Teknolojia na Mawasiliano ndipo **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** alipoona haja ya kuziweka pamoja ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono jitihada za Serikali za kuwaletea maendeleo wananchi wake ikiwemo kurahisisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano nchini kwa kuona umuhimu wa uanzishwaji wa Wizara hii makhsusi ya Mawasiliano, Teknologia ya Habari na Ubunifu ili iweze kusimamia, kukuza na kuimarisha matumizi ya Teknologia ya kisasa na kurahisisha huduma za Serikali ambapo itaongeza ufanisi katika sekta za kiuchumi (kama utalii) na kuhimiza ubunifu wa kidijitali kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii visiwani Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya maono mazuri ya Serikali ya kuanzisha Wizara hii, kamati inaona ipo haja kwa Wizara ya Fedha kuyaangalia vizuri makadirio ya matumizi ya Bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano, Teknologia ya Habari na Ubunifu kwani Bajeti waliokadiriwa kupewa ni kidogo mno ukilinganisha na uhalisia wa utekelezaji wa huduma ambazo zinatarajia kutolewa na Wizara hii na kuweza kufikia malengo ya Serikali yaliokusudiwa kwa ufanisi. Ikiwa katika hatua za kuanzishwa kwake, Wizara hii inahitaji

uwekezaji mkubwa wa kifedha ili iweze kuzihudumia Wizara nyengine zote katika Nyanja za mawasiliano, TEHAMA na Ubunifu.

**Sambamba na hilo** pia kamati inashauri kupatiwa Wizara Jengo la kudumu litakalowaweka pamoja uongozi na taasisi zake zote kwa ajili ya matumizi ya kiofisi kwani Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu hasa ukizingatia zama hizi za kidigitali na mwelekeo wa Serikali kuelekea uchumi wa kidigitali.

## PROGRAMU KUU YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI (TEHAMA) (P01)

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii imeundwa na Programu Ndogo mbili (2), ambazo ni Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA na Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imepanga kutumia jumla ya **Shilingi Milioni Mia Sita Sitini na Nane, Laki Mbili Themanini na Tatu Elfu (668,283,000/-)** sawa na **asilimia 1.25** ya Bajeti ya Wizara. Miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia Programu hii ni kuimarisha miundombinu na huduma bora, salama na za uhakika za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), pamoja na kuhakikisha usalama wa taarifa binafsi na mifumo ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuipatia fedha Program kuu hii kama zilivyokadiriwa kwa mwaka huu wa fedha na

pia kuiongezea makadirio kwa mwaka wa fedha ujao 2027/2028 ili iweze kufikia malengo yake yaliowekwa na kuchochea ukuaji wa ubunifu na mageuzi ya kidijitali, na kupelekea kuongezeka fursa za ajira kupitia sekta ya ubunifu.

**Mheshimiwa Spika,** ZICTIA ni miongoni mwa taasisi muhimu katika taasisi za Serikali ambayo inatoa mchango mkubwa kwa taasisi nyengine za Serikali na binafsi hasa kwenye sekta ya Mawasiliano. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuipatia mtaji wa kutosha shirika hili ili liweze kuboresha miradi yao ikiwemo mji wa TEHAMA Zanzibar. Pia Kamati inaishauri Wizara kupitia shirika kuimarisha mifumo yao ya utowaji huduma kuwa bora na endelevu ili kuwavutia wateja wengi zaidi kutoka nje na ndani ya zanzibar na kuongeza mapato katika mfuko mkuu wa Serikali Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufikia malengo ya uundwaji wa Wizara hii ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya fedha, kuiongezea Bajeti Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2027/2028 ili Wizara iweze kutekeleza majukumu Waliyojipangia ikiwemo utekelezaji wa kifungu kidogo cha miundombinu na huduma za Tehama **(S0101)** kupitia Programu kuu hii ambacho kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kimekadiriwa kutumia **Shilingi Milioni mia mbili Thelathini na nane, Laki Saba Kumi na Nane Elfu (238,718,000/-)** ili kuweza kutekelezeka kazi zake kwa ufanisi

uliokusudiwa, kwani kuwapata wataalaam waliobobea kwenye fani ya Tehama kunahitajika rasilimali fedha zaidi na ya uhakika kutokana na uchache na umuhimu wao. Hivyo kunahitajika Bajeti kubwa zaidi kwa ajili ya kuwaendeleza kielimu pamoja na kuwalipa stahiki zao ili kuwabakisha katika utumishi wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA **(S0102)** inasimamiwa na Idara ya Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Pamoja na Idara ya Ubunifu ambapo lengo lake ni kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa binafsi pamoja na mifumo ya TEHAMA, na kukuza na kushajihisha ubunifu wa TEHAMA kwa kuweka mazingira wezeshi yanayotokana na uwepo wa sera na sheria rafiki. Kamati inashauri suala la Ubunifu litenganishwe na masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi na ifanywe programu ndogo ya kukuza na kuendeleza Ubunifu iwe ni yenye kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika,** katika kukiboresha kifungu cha huduma cha Usimamizi na udhibiti wa maendeleo ya Ubunifu **(H010202)** katika Program hii, Kamati imeona itakua ni jambo la busara zaidi kwa majukumu yaliyokuwa ya **SMIDA** "ambayo miongoni mwa malengo yake ni kuhamasisha matumizi ya Teknolojia na Ubunifu ili kuboresha viwanda vidogo vidogo na wajasiriamali" kuletwa katika Wizara hii ili kuja kufanya kazi pamoja na **COSOZA** "Ambayo inashughulikia masuala ya hakimiliki na haki shirikishi Zanzibar na

miongoni mwa kazi zake zikiwa ni pamoja na kulinda haki za wabunifu na wavumbuzi, kusajili kazi za Sanaa, kusimamia matumizi ya kazi hizo na kuhakikisha wasanii wanapata stahiki zao" ili kufikiwa ile dhana ya Ubunifu iliyokusudiwa na Serikali kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na wageni wanaoishi Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia vikao mbali mbali na Wizara hii, Kamati iliitaka Wizara kulitilia maanani zaidi suala la Ubunifu kwani nchi haiwezi kupata maendelea bila ya kuwa na wabunifu ambao wataisaidia nchi kuzalisha na kubuni vitu mbali mbali kwa maendeleo ya nchi yetu. Kamati imeshauri umuhimu wa kushajiishwa Ubunifu katika kila Sekta ya Uchumi na uzalishaji badala ya kujikita na Ubunifu katika TEHAMA peke yake.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Wizara kupitia kifungu kidogo cha huduma ya usimamizi na uanzishaji wa vituo vya ubunifu **(H010204)** kuhakikisha vituo hivyo vinafanya kazi kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wake kama Kuendeleza Teknologia na ubunifu kwa vijana, kukuza ujasiriamali na Ajira, usimamizi wa taarifa na elimu, kuhimiza ukuaji wa kiuchumi na utekelezaji wa miongozo ya kitaifa kuelekea uchumi wa kidigitali.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kunakuwa na mpangilio mzuri wa utoaji wa huduma bora za mawasiliano nchini, Kamati inaishauri Wizara kupitia wahusika wake kufanya mazungumzo na

makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano hapa Zanzibar juu ya suala la kushirikiana kwenye matumizi ya minara na sio kila kampuni kuweka mnara wake katika eneo hilo hilo kwa lengo la kupunguza utitiri wa minara katika sehemu moja.

Aidha, Kamati inaona ipo haja kwa Wizara kuchukuwa jitihada za makusudi ili kuweza kuondosha changamoto za kimtandao katika maeneo ya visiwa vikubwa na vidogo ili kurahisisha huduma ya mawasiliano kwa wakaazi na wasafiri wa Bahari wanaopita karibu na visiwa hiyvo sambamba na kuondoa malalamiko ya wateja ya kupata huduma hafifu kulingana na thamani ya fedha wanayolipa.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (P02)

**Muheshimiwa Spika,** Program hii ina jumla ya Programu Ndogo tatu (3) ambazo ni: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Program Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti Za Wizara na Program Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba. Katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2026/2027 Programu kuu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Arubaini na Saba, Milioni Mia Tatu na Mbili, Laki moja Sabiini na Saba Elfu (47,302,177,000/-)** sawa na **asilimia 88.60 ya Bajeti ya Wizara**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi** kwa kuteuwa viongozi mbali mbali katika Wizara hii mpyaa ambao wataenda kusimamia utendaji kazi wa Wizara na kuweza kufikia malengo waliojipangia. Hivyo Kamati inawaomba viongozi pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kuwa na mashirikiano mazuri baina yao ili kuimarisha utendaji wa shughuli zao za kila siku na kuweza kufikia malengo ya Serikali ya kuhakikisha huduma bora za mawasiliano, TEHAMA na Ubunifu zinafikiwa kwa ufanisi na kwa ubora wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Wizara husika kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka huu wa fedha, kuwapatia kibali cha uajiri Wizara hii ya Mawasiliano, Teknologia ya Habari na Ubunifu ili kupunguza uhaba wa Wafanyakazi uliopo sasa ambao unapunguza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

## PROGRAMU KUU YA UENDELEZAJI WA MIFUMO YA MAWASILIANO ZANZIBAR (P03)

**Muheshimiwa Spika,** Program kuu hii ya uendeshaji wa mifumo ya mawasiliano Zanzibzr imeundwa na Programu Ndogo moja, ambayo ni Programu Ndogo ya Mifumo ya Serikali Mtandao ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepangiwa kutumia

jumla ya **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne Ishirini na Moja, Laki Tatu na Arubaini Elfu (5,421,340,000/-)** sawa na asilimia **10.15** ya Bajeti ya Wizara ambapo miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia Program hii ni kuimarisha mifumo ya mawasiliano na huduma za kidijitali zinazotolewa na Serikali, ili ziwe jumuishi, salama, zenye ufanisi na zinazopatikana kwa urahisi kwa wananchi na wadau wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeona ni vyema kwa Serikali kupitia Wizara kuiweka Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ili kuiwezesha taasisi hiyo kibajeti na kuweza kupata Wataalamu wa kutosha ambao watajitosheleza kwenye masuala yote ya mifumo ikiwemo kubuni mifumo mipya na kuiweza kuisimamia wenyewe ili kupunguza ghama za uwendeshaji wa matumizi ya mifumo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwe na mpango mkakati makhsusi wa kuhakikisha wataalamu wa ndani wanashiriki na kushirikishwa ipasavyo katika kubuni, kuunda na kusimamia mifumo inayotumika Zanzibar ili kuiwezesha nchi kuwa na wataalamu endelevu kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Wizara kupitia uongozi wa eGAZ kuwasimamia vizuri na kuwapa hamasa na motisha maafisa wanaohusika na uendeshaji na usimamizi wa Mifumo hapa

Zanzibar ili kuhakikisha kuwa wanaondosha kabisa changamoto za mifumo ili iweze kusomana na iweze kufanya kazi kwa usahihi na kuwa endelevu katika utendaji kazi wa kila siku.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Mawasiliano, Teknologia ya Habari na Ubunifu kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, napenda kuchukua fursa hii na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Teknologia ya Habari na Ubunifu kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono Bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

....................................

Mihayo Juma N'hunga,
Mwenyekiti,
Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA,
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**